

**HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA TASAC YA KUMKARIBISHA MGENI  
RASMI MKUU MKOA WA PWANI YA KUFUNGUA MAFUNZO NA MAZOEZI YA  
MPANGO WA TAIFA WA KUJIANDAA NA KUPAMBANA NA UMWAGIKAJI WA  
MAFUTA KWENYE BAHARI NA MAZIWA (NATIONAL MARINE OIL SPILL  
RESPONSE CONTINGENCY PLAN-NMOSRCP)**

**UKUMBI WA ADEM- BAGAMOYO**

**PWANI,**

**TAREHE 20-22 MACHI, 2023**

**Mheshimiwa Abubakari Mussa Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa  
Pwani,**

**Ndugu Wawakilishi wa taasisi mbalimbali za Serikali,**

**Ndugu Wawakilishi wa Makampuni ya Uagizaji wa Mafuta,**

**Ndugu Wawakilishi wa Wavuvi wa Bagamoyo,**

**Ndugu wanahabari,**

**Wageni waalika mabibi na mabwana**

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA  
TANZANIA! .....**

Awali ya yote natoa shukrani za kipekee kwako Mgeni rasmi kwa kukubali ombi letu na kujumuika nasi katika mkutano huu mafunzo haya ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kupambana na Umwagikaji wa Mafuta kwenye Bahari na Maziwa. ambapo zoezi hili linafanyika kwa mara ya kwanza hapa Bagamoyo ikijumuisha Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Tunafahamu kuwa unayo majukumu mengi na makubwa yenye maslahi makubwa kwa Taifa, hata hivyo umeweza kutenga muda na kufika hapa ili kutimiza jukumu hili ambalo pia ni la maslahi makubwa kwa Watanzania na Taifa letu kwa jumla.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Jukumu tunalolifanya hapa leo hii ni kwa mujibu wa Sheria ya TASAC na. 14 ya mwaka 2017 na kanuni ya 11 (1) (g) ya TASAC **ya kusambaza habari na kujenga ufahamu kuhusu masuala ya mazingira ya baharini, Usalama na Ulinzi;** Kwa maana hiyo TASAC kama mdhibiti wa mazingira ya bahari analo jukumu kwa mujibu wa sheria la kusimamia na kulinda utunzaji wa mazingira ya bahari na Maziwa. Jukumu hili la ushirikishwaji wa wadau ni zao la utawala bora ambapo inasisitizwa kushirikisha wadau kwenye utekelezaji wa majukumu ya kiudhibiti ambayo misingi yake imejengwa kwenye Mpango kazi wa Kitaifa wa kupambana na Umwagikaji wa Mafuta Baharini (**National Marine Oil Spill Response Contingency Plan**) wa Mwaka 2020.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mkutano wetu wa leo utakuwa na mawasilisho kutoka kwa wawezeshaji wetu kuhusu Mpango kazi wa Kitaifa wa kupambana na Umwagikaji wa Mafuta Baharini (**National Marine Oil Spill Response Contingency Plan**) na nafasi za ushiriki wa wadau.

Wawezeshaji wetu kwa siku ya leo watapata nafasi ya kutushirikisha kuhusu mgawanyo wa majukumu ya kazi ya kupambana na umwagikaji wa mafuta endapo yatatokea baharini. Mawasilisho haya yataweza kumpa nafasi mdau ya kufahamu sehemu yake ya kazi kwa kushirikiana na wenzake na kufahamu nini cha kufanya.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Natoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliopo hapa kwa kukubali mwaliko wetu na kuhudhuria semina hii. Ninatambua kila mmoja wetu ana majukumu mazito ya kiofisi au binafsi lakini kwa kutambua umuhimu wa semina hii mmeacha shughuli zenu ili kwa pamoja tuweze kushirikiana. Napenda kusema kwa msisitizo kuwa semina hii ni kwa ajili yenu ndugu wadau hivyo mnaombwa kufuatilia kwa umakini na kushiriki vyema.

Niwahakikishie kuwa ushiriki wa kila mmoja wenu hapa ni wa muhimu sana na watalaam wetu hapa wapo pamoja na ninyi kwa kipindi chote cha mafunzo na mazoezi haya

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

TASAC, kwa kutambua kwamba si wadau wote wangeweza kufika hapa imeweka utaratibu wa kuwatembelea wadau wote ambao wamepata uelewa juu ya mafunzo haya na kutaka kufanya mafunzo mengine ya kuwajengea uwezo. Mafunzo hayo yataratibiwa na Halmashauri zetu huku wataalamu wetu wakiwapatia elimu zaidi juu ya uelewa wa mafunzo hayo.

TASAC, inasisitiza kuwa wadau wote baada ya kupata uelewa wa mafunzo hayo watakaporudi katika vituo vyao vya kazi wazidi kutoa elimu hii ambayo ni muhimu kwa wadau wote na wananchi kwa ujumla

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Baada ya kusema hayo, naomba nikukaribishe uongee na hadhara hii, kisha nakuomba utekeleze jukumu kubwa la **kufungua semina hii ya wadau juu ya Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kupambana na Umwagikaji wa Mafuta kwenye Bahari na Maziwa.**

Asanteni kwa kunisikiliza

Kaimu Abdi Mkeyenge.

**Mkurugenzi Mkuu TASAC**